TANGAZO LA SERIKALI Na. 723 la tarehe. 16/8/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU WA MAZIWA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Maziwa ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ya Mwaka 2024.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Pangani;

Sura ya 262

"maziwa" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Tasnia ya Maziwa;

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu, taasisi, kampuni au mashirika yanayojishughulisha na biashara ya maziwa;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji;

"mwenyekiti"-

(a) kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani;

(b) kuhusiana na Kijiji maana yake ni Mwenyekiti wa Kijiji;

(c) kuhusiana na Kitongoji maana yake ni Mwenyekiti wa kitongoji;

"ushuru" maana yake ni tozo ya maziwa itakayotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri.

Vituo vya kukusanyia maziwa

3. Halmashauri itaanzisha vituo vya kukusanyia maziwa katika eneo lote la Halmashauri.

Utozaji wa ushuru

4. -(1) Halmashauri itatoza ushuru wa maziwa kwa kiwango cha asilimia tatu ya bei ya kununulia maziwa katika vituo vya kukusanyia maziwa utakaolipwa na mnunuzi.

(2) Ushuru utalipwa kwa Halmashauri au wakala.

(3) Malipo ya ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ushuru.

(4) Masharti ya kanuni hii hayatumika kwa wauzaji wa maziwa yenye ujazo usiozidi lita kumi wanaouza maziwa yao katika vituo vya kukusanyia maziwa.

Kibali cha kusafirisha maziwa

5.-(1) Mtu yoyote hataruhusiwa kusafirisha maziwa ya biashara nje ya Halmashauri bila kuwa na kibali.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha maziwa kwa mnunuzi kama kilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.

Uteuzi wa Wakala

6.-(1) Halmashauri inaweza kumteua Wakala kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria ndogo hizi;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Rejesta ya wanunuzi wa maziwa

7.-(1) Kutakuwa na rejesta ya wanunuzi wa maziwa kwa kila kituo cha kukusanyia maziwa.

(2) Kila kituo cha kukusanyia maziwa kitatunza rejesta yake ya kutunza kumbukumbu za wanunuzi wa maziwa.

Kutolipia Ushuru wa Maziwa

8.-(1) Endapo mnunuzi atashindwa kulipa ushuru kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ndogo hii, maziwa yatakamatwa na kuhifadhiwa kwa masaa kumi na mbili na baada ya muda huo kupita bila mnunuzi kuyakomboa, maziwa hayo yatauzwa kwa njia ya mnada.

(2) Fedha zitakazopatikana baada ya mauzo ya maziwa yaliyokamatwa na kunadiwa chini ya kanuni ndogo ya (2), Halmashauri itachukua ushuru wake, gharama za utunzaji wa maziwa kwa wakati wote maziwa yalipokuwa chini ya uangalizi wa Halmashauri pamoja na gharama za mnada, kiasi kitakachobaki atarudishiwa mnunuzi.

Maziwa kupoteza thamani

9. Endapo maziwa yaliyokamatwa chini ya kanuni ndogo ya (2) yatapoteza thamani, Halmashauri haitahusika na upotevu wa thamani katika maziwa hayo yaliyopo chini ya uangalizi wake, isipokuwa tu kama kupoteza thamani kumesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Makosa na adhabu

10. Mtu ambaye-

(a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ushuru; na

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi,

anatenda kosa, akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili ikiwa mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ushuru anaodaiwa.

*Tangazo la Serikali Na.723 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2))*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZIWA

Jina la mwombaji …………………………………………………………………
Anwani ya mwombaji……………………………………………………………
Tarehe ya maombi…………………………………………………………………

Kibali kinatolewa kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo kama ulivyoomba kwa mujibu wa Sheria. Kibali hiki ni kwa ajili ya kusafirisha maziwa nje ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

MAELEZO YA MAZIWA YANAYOSAFIRISHWA
NJE YA HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI

Jina la mwenye gari ………………………………………………………………
Jina la dereva ……………………………………………………………………
Sahihi ya dereva …………………………………………………………………
Kiasi cha maziwa yanayosafirishwa (tani/lita) ……………………………………
Sehemu/kampuni/mfugaji/ushirika/mmiliki wa maziwa ……………………………
Hali ya maziwa (*hayajachakatwa, yamechakatwa, ingine taja*) ……………………
Yanakopelekwa/kusanywa …………………………………………………………
Jina la mnunuzi …………………………………………………………………
Aina ya usafiri *(taja pamoja na namba za usajili)* ………………………………

MAONI YA AFISA MWIDHINIWA
Kibali kimetolewa/hakijatolewa (taja sababu) ……………………………………
Ushuru wa maziwa umelipwa/ haujalipwa …………………………………………
Stakabadhi namba ………………………………………………………………
Jina la Afisa Mwidhiniwa …………………………………………………………
Cheo/Wadhifa ……………………………………………………………………
Tarehe ……………………………………………………………………………

(N.B) kibali kijazwe nakala mbili moja apatiwe msafirishaji na nyingine iwasilishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W).

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, kwamba mnamo tarehe...................... ya mwezi...............……. Mwaka...................…… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …..................… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Maziwa ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru na faini ninayodaiwa badala ya kupelekwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. mwezi…………..… mwaka ……….........……….……….

Jina……………………………….. Saini……………………..................………

MBELE YANGU :

Jina:……………………..............……………..……………………
Saini:……………………….……….……………………..………
Wadhifa:…….……………………………………………………
Tarehe; ………………….………………………………………………

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani uliobandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofsanyika mnamo tarehe 29/4/2022 mbele ya:-

ISAYA MUGISHAGWE MBENJE,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Pangani*

AKIDA OMARI BAHORERA,
*Mwenyekiti*,
*Halmashauri ya wilaya,*
*Pangani*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
30 Novemba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb.),
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*,